JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# SERA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA

Wizara ya Maendeleo ya Jamii
Wanawake na Watoto
S.L.P. 3448, Dar es Salaam
TANZANIA

MWAKA 2000

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# SERA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii**
**Wanawake na Watoto**
**S.L.P. 3448, Dar es Salaam**
**TANZANIA**

**Mwaka 2000**

## YALIYOMO


UKURASA

YALIYOMO i
VIFUPISHO iii
DIBAJI iv

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .................. 1
Dhana za Maendeleo ya Jamii, Wanawake katika Maendeleo na Jinsia ......................... 3
Dhana ya Maendeleo ya Jamii ...................... 3
Dhana ya Wanawake katika Maendeleo ........... 3
Dhana ya Jinsia ...................................... 4
Nafasi ya Wanawake katika Jamii ya Tanzania .. 4
Malengo ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ............................................. 5
Madhumuni ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ................................. 7

**SURA YA PILI: HALI HALISI YA WANAWAKE** ...... 10
Hali ya Wanawake Kiuchumi ....................... 10
Mikakati ya Kuondoa Umaskini ..................... 12
Mikakati ya Matumizi Bora ya Rasilimali na Nyenzo ........................................... 12
Hali ya Wanawake katika Jamii ................... 13
Mikakati ya Mila na Desturi ........................ 14
Afya ya Wanawake na Uzazi Bora ................ 15
Mikakati ya Kuimarisha Lishe Bora na Afya ya Familia ............................................ 15
Wanawake na Mazingira ........................... 16
Mikakati ya Hifadhi ya Mazingira ................. 16
Hali ya Elimu, Mafunzo na Ajira kwa wanawake ............................................ 16

Mikakati ya Elimu .................................. 18
Mikakati Juu ya Ajira ............................. 20
Hali ya Wanawake katika Kufanya
Maamuzi ............................................ 21
Mikakati ya Ushirikishwaji ......................... 22
Haki za Wanawake .................................. 23
Mikakati ya Utekelezaji wa Haki za
Wanawake ........................................... 23
Hali ya Hifadhi ya Jamii .......................... 25
Mikakati ya Hifadhi ya Jamii ...................... 25
Wingi na Uzito wa Kazi Walizonazo
Wanawake .......................................... 25
Mikakati ya Kuwapunguzia Uzito wa Kazi ....... 26

**SURA YA TATU: WAHUSIKA KATIKA KULETA MAENDELEO YANAYOZINGATIA USAWA WA JINSIA ............................................ 28**
Jamii Yenyewe ...................................... 29
Serikali ............................................. 32
Wahisani ............................................ 35
Mashirika ya yasiyo ya Kiserikali, ya Hiari,
Wahisani na Taasisi Nyingine ..................... 35

**SURA YA NNE: UTEKELEZAJI WA SERA ......... 37**
Utekelezaji wa Jumla wa Sera ya Maendeleo ya
Wanawake na Jinsia ................................ 37

**SURA YA TANO: MFUMO WA URATIBU NA USIMAMIZI WA MASUALA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA .......................... 39**
Mwisho ............................................... 41

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| CEDAW | - | Convention on the Elimination of all Forms of Discrimination Against Women |
| EOTF | - | Equal Opportunities for All Trust Fund |
| IDM | - | Institute of Development Management |
| IFM | - | Institute of Finance Management |
| NGO | - | Non Governmental Organisation |
| NIC | - | National Insurance Company |
| NPF | - | National Provident Fund |
| NSSF | - | National Social Security Fund |
| OUT | - | Open University of Tanzania |
| PPF | - | Parastatal Pension Fund |
| TAHEA | - | Tanzania Home Economics Association |
| TANGO | - | Tanzania Association of Non Governmental Organisations |
| TAWLA | - | Tanzania Women Lawyers' Association |
| TAMWA | - | Tanzania Media Women's Association |
| TGNP | - | Tanzania Gender Networking Programme |
| WLAC | - | Women's Legal Aid Centre |
| UDSM | - | University of Dar es Salaam |
| VMW | - | Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi |

## DIBAJI

Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni mojawapo ya miongozo ya serikali katika jitihada za kuwapa wananchi mwelekeo wa maendeleo ya wanawake na jinsia utakaohakikisha kuwa Sera, Mipango, Mikakati na Shughuli mbalimbali za maendeleo katika kila sekta na taasisi katika ngazi zote zinazingatia usawa wa jinsia. Sera hii inachukuwa nafasi ya Sera ya Wanawake Katika Maendeleo ya mwaka 1992 ili kuingiza dhana ya Jinsia katika maendeleo ya jamii. Dhana ya Jinsia ni mtazamo mpya wa kuharakisha maendeleo kwa kuangalia mahusiano ya jamii kati ya wanawake na wanaume ambayo yanatambua tofauti zilizopo za kijinsi (sex) baina yao pamoja na mgawanyo wa majukumu katika jamii. Ili kuweza kupata maendeleo ya haraka na endelevu dhana ya Jinsia pia inatilia mkazo umuhimu wa kushirikiana na kufanya kazi kwa kutegemeana kati ya wanawake na wanaume. Hii inatokana na ukweli kuwa majukumu ya wanawake katika jamii ni tofauti na yale ya wanaume na kuwa yote ni muhimu kwa maendeleo ya familia, jamii na Taifa.

Aidha dhana hii ina lengo la kutambua mahitaji ya wanawake na wanaume katika kutekeleza majukumu yao.

Mwelekeo wa maendeleo ki-jamii, ki-taifa na ki-mataifa hivi sasa unasisitiza na kuhimiza upangaji na utekelezaji mipango unaozingatia ushirikishwaji wa

wanawake na wanaume kwa pamoja katika kutambua, kuthamini na kukuza vizuri zaidi uwezo wa wananchi katika kujiletea maendeleo yao. Utekelezaji wa Sera hii utazingatia mchango wa sekta mbalimbali za serikali na zisizo za serikali, waatalam mbalimbali wakiwemo wasomi na wanataaluma na watu binafsi wanawake na wanaume. Msukumo utalenga katika kuingiza masuala ya Jinsia (Gender Mainstreaming) na kuhakikisha kuweko kwa shughuli mbalimbali zinazowalenga wanawake (Women Specific) ili kuharakisha kuwepo usawa wa kijinsia unaotarajiwa.

Ili kurahisisha na kuwezesha utekelezaji, Sera imeelekeza kuwepo na vitengo vya Jinsia (Gender Focal Points) katika muundo wa serikali kuu na serikali za mitaa na taasisi mbalimbali. Vile vile Sera inasisitiza umuhimu wa kuwepo kwa chombo kisichofungamana na itikadi yoyote cha kuwaunganisha wanawake na kuishauri serikali.

Napenda kuzishukuru taasisi zote na wote walioshirikiana na Wizara yangu kukamilisha kazi hii. Aidha, napenda kutoa shurkani maalum kwa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD) na Serikali ya Ireland kwa mchango wao uliowezesha kazi hii kufanyika.

Ni matumaini yangu kwamba Sera hii itatumika katika utayarishaji, uandaaji na utekelezaji wa Sera

mbalimbali za Taifa na sekta ili kuhakikisha maendeleo ya wanawake na jinsia yanapatikana.

Mary M. Nagu (Mb)

**Waziri wa Maendeleo ya Jamii,**
**Wanawake na Watoto.**

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

1. Sera ya Maendeleo ya Wanawake katika Maendeleo ilipitishwa na kuanza kuteke-lezwa mwaka 1992. Sera hiyo ilibuniwa katika misingi ya Dhana ya Wanawake katika Maendeleo.

2. Yapo mafanikio mengi yaliyopatikana katika utekelezaji wa Sera hiyo ingawa ushiriki wa wanaume haukujitokeza vya kutosha. Mafanikio yaliyopatikana ni, kama vile, kuwepo kwa ufahamu zaidi kuhusu haki za wanawake katika ngazi mbali mbali za kufanya maamuzi na mipango; uanzishwaji wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayolenga kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika nyanja mbalimbali, kutambulika kwa michango ya wanawake katika maendeleo yote ya nchi; na wanawake kupewa fursa zaidi katika nyanja mbali mbali zikiwemo za siasa, uongozi, utawala, na kujiletea maendeleo ya kiuchumi.

3. Pamoja na mafanikio hayo ni dhahiri kuwa jamii, bado haijawa na mwelekeo wa kusawazisha tofauti za kijinsia zilizopo baina ya wanawake na wanaume; na hivyo marekebisho yaliyomo katika Sera hii yanalenga katika kuweka mikakati, programu na miradi mbalimbali itakayo-harakisha kuziba pengo la kijinsia katika maeneo

karibu yote ya maendeleo, haki na usawa, na hivyo kuleta mazingira bora zaidi ya ushiriki wa wanawake katika maendeleo. Aidha, Sera pia inaelekeza jinsi wanaume na wanawake watakavyotimiza wajibu wao kufuatana na mahitaji ya kijinsia na hatua mbalimbali watakazochukua ili kuhakikisha fursa sawa, haki na usawa kwa wote. Vile vile sera inaelezea majukumu ya wahusika katika utekelezaji wake pamoja na mfumo wa uratibu na usimamizi wake.

4. Tanzania ni nchi inayothamini usawa na haki za binadamu. Imani hii imeelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa mwaka 1984. Katiba hii inasisitiza usawa na heshima kwa binadamu wote, heshima ya kutambua na kuthamini utu wa mtu pamoja na kuhakikisha haki mbele ya sheria.

5. Katiba (kifungu cha tatu) inalinda uhuru wa mtu mwanamume au mwanamke kupata hifadhi ya maisha, kumiliki mali na pato la jasho lake, kufanya kazi na kupata haki ya kujielimisha kufikia upeo wake. Kwa kifupi inataka kuwepo kwa jamii yenye usawa, haki, uhuru na fursa sawa kwa watu wote kuweza kushiriki na kutumia kwa ukamilifu uwezo na vipaji walivyonavyo katika shughuli za umma, uongozi wa nchi, utamaduni, uzalishaji mali na upatikanaji wa huduma za jamii ili wapate kuendelea na kuwa na hali bora zaidi ya maisha yao na taifa lao.

6. Kutokana na msimamo huu Tanzania imekwishatia saini Tamko la Umoja wa Mataifa kukiri imani yake kuwa binadamu wote ni sawa na wana haki sawa mbele ya sheria na katika kugawiwa rasilimali au huduma mbali mbali za jamii. Aidha Tanzania imetia saini Mkataba wa Nchi Huru za Afrika unaotambua haki za binadamu wote, vile vile imeridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi na Uonevu kwa Wanawake.

**Dhana za Maendeleo ya Jamii, Wanawake katika Maendeleo na Jinsia :**

**Dhana ya Maendeleo ya Jamii**

7. Maendeleo ya Jamii kama dhana ni hatua zinazowawezesha "watu" kutambua uwezo walio nao wa kubaini matatizo na uwezo wao wa kutumia rasilimali zilizopo kujitatulia matatizo hayo, kujipatia na kujiongezea kipato na kujiletea maisha bora zaidi na hivyo kwa ujumla, kujiletea maendeleo.

**Dhana ya Wanawake Katika Maendeleo**

8. Dhana ya wanawake katika maendeleo inatafsiriwa kuwa ni hatua madhubuti za kujenga uwezo wa wanawake kujitegemea katika kufanya maamuzi juu ya maisha yao na kutekeleza maamuzi hayo kwa kutumia rasilimali zilizopo bila kuingiliwa au kubughudhiwa na mtu, taasisi

au chombo chochote kwa sababu tu wao ni wanawake.

**Dhana ya Jinsia**

9. Jinsi ni maumbile ya wanawake na wanaume. Majukumu ya wanawake yatokanayo na jinsi zao ni kuzaa na kunyonyesha watoto wakati wanaume wakiwa na majukumu tofauti na hayo. Dhana ya Jinsia, ni mahusiano kati ya wanawake na wanaume yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa na jamii pamoja na kutambua tofauti zao za kimaumbile, mgawanyo wa majukumu ya kazi, mgawanyo wa mapato na rasilimali nyingine, fursa sawa za kushiriki katika siasa na utawala, mila na desturi mbali mbali n.k. Dhana ya Jinsia inalenga katika kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake katika maeneo yote yanayohusu haki, amani na maendeleo ya kiuchumi, kijamii kiutamaduni na kisiasa.

**Nafasi ya Wanawake katika Jamii za Tanzania**

10. Ingawa kwa ujumla jamii za Tanzania, kama zilivyoainishwa kwenye Sera ya Maendeleo ya Jamii hazijatumia uhuru, fursa na haki kikamilifu katika kujiletea maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii n.k., hali hiyo ni mbaya zaidi kwa wanawake kutokana na sababu mbali mbali ambazo zimechangia kuwabagua ikilinganishwa na wanaume.

11. Katika mazingira haya wanawake hawajitokezi kiasi cha kutosha kugombea nafasi za uongozi na kwa jumla, hawashiriki vya kutosha katika kutoa maamuzi katika ngazi mbali mbali, kuanzia familia hadi ngazi ya Taifa. Wanawake na hasa wa vijijini wanaofanya kazi ni asilimia 80 ya nguvu kazi iliyopo vijijini na huzalisha asilimia 60 ya chakula chote. Ingawa wao ndiyo wazalishaji mali wakuu, mazingira haya yanawafanya wasiwe na uamuzi wa mwisho hata juu ya mali waliyozalisha wao wenyewe. Hali kadhalika katika masuala ya uzazi wanawake hawana maamuzi. Kwa mfano, hawana maamuzi juu ya idadi ya watoto katika familia ingawa wao ni wazazi na wana jukumu kubwa zaidi la ulezi wa watoto hao.

**Malengo ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia:**

12. Lengo kuu la Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni kuweka mazingira muafaka yatakayowawezesha wanawake na wanaume kutekeleza majukumu yao katika jamii kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia. Aidha Sera hii inalenga katika kusawazisha mapungufu yanayojitokeza katika ushirikishwaji wa wanawake katika shughuli za maendeleo. Sera inawawezesha wanawake wa Tanzania kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika kutambua uwezo wao wa kubaini matatizo na kuyatatua kwa kutumia rasilimali zilizopo, ili kujiongezea kipato

na kuondoa umasikini kwa ujumla na hivyo kujiletea maisha bora zaidi. Hii ni pamoja na uwezo wa kufanya maamuzi katika nyanja mbalimbali na kuyatekeleza. Aidha Sera imetia maanani kuwa katika kufikia azma hiyo, wanaume hawana budi kutekeleza wajibu wao barabara katika jamii zetu na hivyo kushirikiana na wanawake katika majukumu mbalimbali ya kijamii na kiuchumi.

13. Malengo mahsusi ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni:

(a) Kuwawezesha wanawake, wanaume na jamii yote kulitafakari kwa kina tatizo la umaskini na hivyo kuliwekea mikakati thabiti ya kukabiliana nalo.

(b) Kuiwezesha jamii wakiwemo wanawake na wanaume kutumia zaidi mali zao katika mambo yatakayowaletea maendeleo.

(c) Kuiwezesha jamii ya Watanzania kuitekeleza kwa dhati imani yao ya Ki-taifa ya kuwepo Usawa na Haki miongoni mwa wananchi bila kuwepo tofauti za ki-jinsia na hivyo kuweka mazingira muafaka ya kuongeza kasi ya maendeleo.

(d) Kuiwezesha jamii ya Watanzania, kuuona bayana, na kuupa thamani inayostahili, mchango wa wanawake katika maendeleo

yao, ya familia zao na ya Taifa, kwa ujumla, na kutambua haki zao katika maendeleo hayo katika ngazi zote.

(e) Kuiwezesha jamii kuona umuhimu wa wazazi wote wawili (baba na mama) kushiriki kikamilifu katika malezi ya watoto.

**Madhumuni ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia**

14. Madhumuni ya Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ni kutoa mwelekeo utakaohakikisha kuwa mipango, mikakati na shughuli mbali mbali za uongozi na maendeleo katika kila sekta na taasisi inazingatia usawa wa kijinsia. Madhumuni maalum ya Sera yatajumuisha:

(a) Kutoa miongozo mbali mbali itakayohakikisha kuwa mipango ya maendeleo inazingatia usawa wa kijinsia.

(b) Kutoa tafsiri sahihi ya dhana za Jinsia na Wanawake katika Maendeleo na jinsi zinavyooana na dhana ya Maendeleo ya Jamii.

(c) Kuhakikisha kuwepo kwa ushirikiano wa makusudi, wa kudumu na wa karibu kati ya mamlaka zote zinazohusika na kuendesha, kuendeleza na kusimamia maendeleo ya jamii katika:

(i) Kupanga na kutekeleza mipango itakayozingatia jinsia.
(ii) Kutayarisha na kusimamia bajeti ya matumizi ya kawaida na ya mipango ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa inalenga katika kuwaondoa wanawake na jamii kwa ujumla kutoka katika hali duni.
(iii) Kuhakikisha kuwa Sera za Jumla za Uchumi zinalenga katika kukabili matatizo maalum ya wanawake, wanaume na jamii kwa jumla.

(d) Kuelimisha jamii kutambua na kusisitiza kuwa usawa wa kijinsia utapatikana tu utakapokuwa na mizizi thabiti ndani ya familia na kaya za jamii za Watanzania.

(e) Kuweka mazingira mazuri ya kisheria yatakayohakikisha kuwa hapata-kuwepo na sheria zenye ubaguzi wa kijinsia, ziwe za Serikali au Kimila.

(f) Kuelimisha jamii kuwa uharibifu wa mazingira umekuwa chanzo kikubwa cha kuwaongezea wanawake mzigo wa kazi hususan katika kutafuta kuni na kutafuta maji, kadhalika kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika mipango na programu zinazoendeleza hifadhi ya mazingira.

(g) Kuelimisha jamii kuona umuhimu wa malezi

bora ya watoto na vijana ili siku za usoni kusiwepo ubaguzi wa kijinsia.

(h) Kuainisha majukumu ya wanawake na wanaume vizuri ili wote waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo kwa manufaa ya jamii.

(i) Kuweka bayana vigezo vya kupima mafanikio ya juhudi za Taifa za kuleta usawa kijinsia.

(j) Kuanzisha na kuboresha vitengo vya wanawake na jinsia katika kila sekta nchini.

(k) Kuanzishwa kwa chombo cha wanawake cha kuratibu shughuli za vyama, mashirika na jumuiya za wanawake kwa lengo la kushauri serikali ipasavyo.

## SURA YA PILI

## HALI HALISI YA WANAWAKE

15. Kwa miaka mingi, hapa nchini idadi ya wanawake imekuwa ni kubwa asilimia 52 kuliko ile ya wanaume ambayo ni asilimia 48 Ingawa idadi kubwa (asilimia 75) ya watu iko vijijini, katika wakati wowote wanaume wengi wako mijini. Hali hii inajitokeza kutokana na kazi na biashara ambazo wanaume hupendelea kuzifanya. Hali hii pia inatokana na fikra potofu kuwa kilimo ni shughuli duni na hivyo kuachiwa wanawake zaidi. Kutokana na Sensa ya miongo miwili iliyopita, muundo wa jamii unaonyesha idadi kubwa, asilimia 45 , ni ya vijana walio chini ya miaka 45. Kati yao, asilimia 50 ni wanawake.

### Hali ya Wanawake Kiuchumi:

16. Shughuli za wanawake zinategemea mahali walipo kijiografia, umri wao, mila na destruri za hapo walipo, viwango vyao vya elimu na rasilimali zilizopo. Hata hivyo wanawake kwa kawaida hujihusisha na shughuli zifuatazo:-

(a) Wanawake wengi asilimia (90.4) ni wazalishaji mali katika sekta za kilimo, ufugaji na uvuvi, uchimbaji madini (asilimia 0.1); viwanda vidogo vidogo (asilimia 1.2) na ujenzi (asilimia 0.1). Wanawake katika sekta

ya kilimo wanakabiliwa na tatizo la nyenzo duni, ukosefu wa mitaji, ujuzi mdogo na kutokuwa na milki ya ardhi.

(b) Wanawake (asilimia 44.1) katika miji wanajishughulisha na biashara ndogo ndogo kama vile uuzaji wa nguo, vyakula, vinywaji baridi na vileo. Ingawa wanawake hawa wamejiajiri katika sekta hii ya biashara bado wanakabiliwa na matatizo mengi ya uendeshaji. Matatizo hayo ni ukosefu wa mitaji, nyenzo, masoko, utaalam, ujuzi na maeneo yanayofaa kwa biashara hizo. Ingawa matatizo katika sekta ya biashara ndogo ndogo yanawakabili pia wanaume, wanawake wanaathirika zaidi.

(c) Idadi ya wanawake walioajiriwa katika Serikali, taasisi za umma na za binafsi ni asilimia 32 (1997) tu ya waajiriwa wote katika sekta hizo. Hii ni sehemu ndogo tu ya wanawake. Kwa ujumla asilimia 19 tu ndio wanashika nafasi za kati na juu serikalini na waliobakia kushika nafasi za chini. Aidha kutokana na sera za urekebishaji uchumi na mifumo, wanawake wengi katika Serikali na Sekta ya Umma wameachishwa kazi na kulazimika kuingia katika sekta isiyo rasmi.

## Mikakati ya Kuondoa Umaskini

17. Ili mipango ya kuondoa umaskini iweze kufanikiwa kunahitajika kufufua ari ya wananchi kwa kuwashirikisha katika kubuni na kutekeleza mipango ya kujiletea maendeleo yao wenyewe badala ya kutegemea Serikali. Wahusika wakuu ni wananchi wote katika jamii. Jukumu la Serikali ni kuwezesha nguvu za wananchi kwa kutumia mikakati ifuatayo:-

- Kuelewa chanzo cha umaskini katika jamii.
- Kuelimisha jamii juu ya matumizi bora ya raslimali ambazo zinapatikana ndani ya jamii k.m. muda, ardhi, mifugo, misitu, mito, utaalamu n.k. na vitu vinavyopatikana nje kwa mfano pembejeo za kilimo, mitambo ya viwanda n.k.
- Serikali kuimarisha mifuko ya mikopo nafuu ili kuinua hali ya uchumi wa wanawake na wanaume wenye kipato cha chini.

## Mikakati ya Matumizi Bora ya Rasilimali na Nyenzo

18. Ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali itabidi:-

- Sekta zinazohusika na kupima, kumilikisha ardhi kwa jamii vijijini zihakikishe kuwa wanawake wanapata huduma hiyo ili kuwa na uhakikika wa kutumia na kuweza kujiombea mikopo ya kilimo kwa maendeleo yao na taifa

kwa jumla.

- Kuweka mazingira mazuri ya kilimo na kuhakikisha wakulima wanapata ardhi ya kutosha na pembejeo kwa wakati muafaka.
- Kuongeza upatikanaji wa vitendea kazi na pembejeo na kutumia mbolea za asili.
- Kuimarisha na kuboresha masoko ya wakulima kulingana na mazao wanayozalisha.
- Kuimarisha njia za mawasiliano na hasa vijijini kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za jamii na usafirishaji wa mazao ya kilimo na yatokanayo na misitu.

**Hali ya Wanawake katika Jamii**

19. Kutokana na mila na desturi zilizopo katika jamii zetu wanawake ndio wenye jukumu kubwa la kutunza familia. Mabadiliko ya mfumo wa maisha katika jamii zetu ikichangiwa na hali ngumu ya uchumi, yanafanya jukumu hilo kuwa gumu zaidi na hivyo kusababisha muda mwingi wa wanawake kutumika katika kutafuta mahitaji ya familia zao, na hivyo kubaki na muda mchache sana wa kufanya shughuli za maendeleo, kujipumzisha na kulea watoto. Utafiti umeonyesha kuwa wanawake wanafanya kazi kwa saa 16 hadi 18 kwa siku

20. Mabadiliko ambayo yanatokana na mfumo wa uchumi wa soko huria yamesababisha wanaume wengi kuhama vijijini na kwenda maeneo

mengine kutafuta kazi. Hii imesababisha kuongezeka kwa idadi ya kaya ambazo zinaongozwa na wanawake vijijini. Hii maana yake ni ongezeko kubwa zaidi la kazi za kilimo, kutafuta kuni, kuchota maji na hata kufanya biashara ndogo ndogo kwa upande wa wanawake ili kukidhi mahitaji ya familia zao. Takwimu zinaonyesha kuwa umaskini umeshamiri zaidi katika kaya zinazoongozwa na wanawake ambazo kwa wastani ni asilimia 24 ya kaya zote hapa nchini.

**Mikakati ya Mila na Desturi**

21. Athari hizo zitaondelewa kwa kutilia mkazo mkubwa katika:-

- Kuhamasisha jamii kuacha mila na desturi potofu kama vile kukeketa au kutahiri wanawake;
- Kuhamasisha wanawake na wanaume kupanga uzazi kulingana na uwezo wao wa kuwatunza na kuwaendelea watoto wao; na
- Kuelimisha jamii kuzingatia uzazi wa mpango ili kutoa muda wa kutosha kwa wanawake wa kunyonyesha, na kupumzika na pia kushiriki katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi vizuri zaidi.

### Afya ya Wanawake na Uzazi Bora

22. Ingawa inakisiwa kuwa, kwa wastani wanawake huishi miaka mingi zaidi ya wanaume, umaskini, mila na desturi zilizopitwa na wakati zinasababisha hali ya afya ya wanawake kuwa duni zaidi kuliko ya wanaume. Hali hii inatokana na kuzaa watoto wengi bila kuzingatia uzazi wa mpango, kufanya kazi nyingi na ngumu, kukosa huduma bora za afya na kinga, kukeketwa na, kukosa lishe bora. Baadhi ya athari zinazoweza kutokea kutokana na hali hiyo ni:

    (i) Kudumaa, upungufu wa damu na kuzaa watoto njiti.
    (ii) Maradhi na vifo kutokana na magonjwa kama vile UKIMWI au kupoteza damu nyingi wakati wa uzazi na wakati wa kukeketwa.

### Mikakati ya Kuimarisha Lishe Bora na Afya ya Familia

23. Pamoja na mikakati inayohusu mila na desturi iliyotajwa hapo juu, mkazo pia utawekwa katika:-
    - Kuendeleza teknolojia ya uhakiki wa chakula
    - Kuimarisha programu za mafunzo ya lishe bora kwa wanawake na jamii kama njia ya kinga ya magonjwa.
    - Kila familia kuhakikisha inahifadhi chakula cha kutosha na kuuza ziada tu.

- Kuimarisha huduma za afya na uzazi na kuhamasisha wanawake kupima afya zao kila wakati ili kukidhi mahitaji ya afya bora ya uzazi.

**Wanawake na Mazingira**

24. Aidha ongezeko la jangwa linalotokana na uharibifu wa misitu, kutoweka kwa viumbe na uchafuzi wa maji kutokana na matumizi mabaya ya mazingira, ni vitu vinavyo-mwongezea mwanamke ugumu wa kazi. Athari zake zinamgusa mwanamke kwa kupata mavuno kidogo ya kilimo, kutembea mwendo mrefu zaidi kufuata maji na kutafuta kuni.

**Mikakati ya Hifadhi ya Mazingira**

25. Kuhamasisha wahusika katika ngazi zote juu ya umuhimu wa uwiano wa kijinsia katika kuunda kamati za kuhifadhi mazingira ili kuhusisha kikamilifu wanawake kulinda na kutunza mazingira yanayowazunguka.

**Hali ya Elimu, Mafunzo na Ajira kwa Wanawake.**

26. Kisheria hakuna ubaguzi wowote katika utoaji elimu. Hii inadhihirishwa na idadi inayowiana ya wasichana na wavulana katika elimu ya msingi. Takwimu za Hali ya Uchumi wa Taifa, 1997 zinaonyesha kuwa kuanzia mwaka 1990 hadi 1997 idadi ya wasichana katika shule za Sekondari

nchini imeongezeka kutoka asilimia 41.52 hadi 44.41 ya wanafunzi wote walioingia katika shule za Sekondari. Aidha, takwimu hizo zinaonyesha pia kuwa katika shule za Sekondari zisizo za Serikali wasichana wamekuwa wengi zaidi ya wavulana katika kipindi hicho. Mathalani, mwaka 1990 wasichana walikuwa asilimia 57.36 ya wanafunzi wote waliokuwa katika shule hizo. Tofauti na madai kuwa wazazi hawathamini elimu ya watoto wao wa kike, takwimu hizi zinaonyesha kuwa ingawa wasichana hawapati fursa kubwa kuingia katika shule za Sekondari za serikali, wazazi wao huwapatia elimu hiyo kupitia shule za Sekondari za binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali au shule za jumuiya kama vile za wazazi.

27. Uwiano wa wasichana na wavulana ni mbaya katika shule za Sekondari za Serikali kwa kuwa viwango vya kufaulu vya wasichana viko chini vikilinganishwa na vya wavulana. Hali hii inatokana na sababu mbali mbali zikiwemo kukosa muda wa kutosha wa kujisomea kwa wasichana ambao wako shule za kutwa, kwa kuwa warudipo nyumbani hujishughulisha na kazi za nyumbani, na pia huweza kudanganywa na wanaume kwa kupatiwa zawadi za anasa au vivutio mbalimbali na hivyo kujiingiza katika mapenzi kabla ya wakati wao kufikia, kukosa msukumo wa kutosha kutoka kwa wazazi, na kukosa huduma za msingi kama vile sare, n.k

28. Uwiano wa wasichana na wavulana katika elimu ya juu ni mbaya zaidi. Takwimu kutoka katika Hali ya Uchumi wa Taifa, 1997 zinaonyesha wanawake waliokuwa katika Vyuo Vikuu hapa nchini mwaka 1993/94 na 1997/98 kama ifuatavyo; SUA asilimia 21.17 na 26.84; UDSM asilimia 14.47 na 17.76; Muhimbili asilimia 33.84 na 28.98 OUT (Open University of Tanzania) asilimia 10.05 na 11.60. Ingawa takwimu kwa Vyuo vingine vya elimu ya juu kama vile IDM, IFM, Vyuo Vikuu vya Taasisi za Dini na vile vya nje ya nchi hazikuonyeshwa, hata huko hali haitegemewi kuwa tofauti sana. Sababu za msingi za hali hiyo ni kama zilivyokwishafafanuliwa. Hii inamaanisha kuwa nafasi nyingi za kitaalamu zitaendelea kushikwa na wanaume katika siku za usoni.

**Mikakati ya Elimu**

29. Katika jitihada za kuondoa hali hizo, ni lazima elimu iwe ni nyenzo ya kuondoa ubaguzi wa aina zote katika jamii. Sera ya Elimu ihakikishe kuwa wasichana sio tu wanapata nafasi sawa kuingia katika mfumo wa elimu lakini pia wawezeshwe kuzitumia nafasi hizo kwa ukamilifu. Kwa hiyo sera izingatie mahitaji maalumu ya wanafunzi wa kike kwa kuangalia vigezo muhimu kama vile:-

(i) Udahili - idadi ya nafasi za wasichana katika shule za sekondari na vyuo ziongezwe ili waweze kudahiliwa

wasichana wengi zaidi.

(ii) Kupukutika (to drop out) - Zichukuliwe hatua madhubuti za kupunguza kupukutika kwa wasichana na kukabiliana na sababu kama vile mimba, kuolewa,kushindwa kulipa ada, kukosa nafasi za bweni, kuishi mbali na shule, kukosa usalama au hifadhi shuleni au kushindwa masomo. Ujenzi wa bweni za wasichana katika shule uhimizwe.

(iii) Muhtasari - Kutunga mihtasari ambayo sio tu kuwa itawavutia wasichana kimaendeleo na masomo, lakini pia itakayowapa stadi zitakazowawezesha kujipatia kipato cha kujikimu kimaisha na kuwawezesha kuchangia katika maendeleo ya taifa.

(iv) Hisabati - Sayansi na Teknolojia - kuongeza idadi ya wasichana katika fani hizi na kuwawezesha kuzipenda na kuzimudu, kwani hizi ndiyo funguo za maendeleo katika karne zijazo.

(v) Elimu kwa wazazi - Kuelimisha jamii hasa wazazi kuwa na nafasi sawa kwa wasichana na wavulana katika elimu haitoshi kama hawapati nafasi sawa nyumbani.

(vi) Mikakati mingine katika kuendeleza elimu - Kuanzisha mfuko kwa ajili ya wasichana wenye vipaji vya kuendelea na masomo ya juu .

(vii) Sekta inayohusika iimarishe programu ya

elimu ya watu wazima kwa madhumuni ya kuiwezesha jamii kupata stadi mbali mbali k.m. kupitia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs).

(viii) Kuhamasisha jamii kushiriki katika ujenzi na ukarabati wa majengo ya shule pamoja na ulinzi wa mali za shule.

(ix) Kuhamasisha mashirika yenye uwezo yasiyo ya Kiserikali k.m. Mashirika ya dini kuanzisha na kutoa elimu katika ngazi zote.

(x) Kuhamasisha wanawake na wasichana kujiunga na Vyuo Vikuu ili kupata elimu ya juu zaidi.

30. **Mikakati Juu ya Ajira**

(i) Kuwepo na takwimu sahihi zinazoonyesha idadi kamili ya wanawake na wanaume katika ngazi zote ili kutoa nafasi sawa kutegemea sifa zinazotakiwa.

(ii) Kuwepo utaratibu maalum (wenye urasimu mdogo) katika utoaji wa leseni kwa wafanya biashara ndogo ndogo na hasa kwa wahusika wa sekta isiyo rasmi ambayo wanawake wengi wanajihusisha nayo.

**Hali ya Wanawake katika Kufanya Maamuzi.**

31. Kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa chini ya mfumo wa siasa wa Demokrasia ya Chama kimoja. Wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika kazi ya uhamasishaji umma, lakini wamekuwa wakishiriki kwa kiwango kidogo tu katika maamuzi ya kisiasa. Usawa wa kijinsia utaongeza mahusiano mazuri baina ya wanawake na wanaume na utawaongezea wanawake uwezo wa kujiajiri na hivyo kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za maendeleo ya jamii na uchumi.

32. Hata hivyo ni wanawake wachache tu ambao hujitokeza katika uongozi na uwakilishi katika Bunge na vyombo vingine vya kutoa maamuzi. Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa idadi ya wanawake Wabunge ni asilimia 16, na Wanawake mawaziri asilimia 11 tu (1999).

33. Hali hii inasababishwa na mambo mengi, kama vile wanawake kukosa mbinu za kisiasa, kutojiamini, jamii kutothamini uongozi wa wanawake katika uwanja wa siasa n.k. Kwa kuzingatia ukweli huo na nia njema ya wanawake kushiriki katika vyombo mbali mbali vya kufanya maamuzi, serikali mwaka 1992 ilitenga viti maalum vya wanawake katika Bunge; Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Serikali za Vijiji. Idadi ya Wanawake katika vyombo vya Serikali za Mitaa ni asilimia 25 na katika Bunge la

Jamhuri ya Muungano ilifikia asilimia 15. Aidha baada ya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika mwaka 2000 nafasi za viti vya wanawake katika Bunge zimeongezwa hadi asilimia 20, na aslimia 33 katika Serikali za Mitaa. Kiasi hicho bado ni kidogo ikilinganishwa na matarajio na lengo la kuhakikisha asilimia 30 katika ngazi zote ifikapo mwaka 2005.

### Mikakati ya Ushirikishwaji

34. Katika hali kama hiyo ushirikishwaji wa wanawake na wanaume katika maendeleo ufanyike kama ifuatavyo:-

- Kuhakikisha kwamba mchango wa wanawake katika maendeleo ya taifa unatambuliwa na kuthaminiwa.
- Kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wote wanachangia kikamilifu katika jitihada za maendeleo.
- Kuhamasisha ili takwimu za wanawake na wanaume katika kila ngazi ya uongozi na kazi zionekane bayana na rasilimali zigawiwe kwa kuzingatia jinsia.
- Kuhamasisha wanawake na wanaume washirikishwe katika kupanga na kusimamia matumizi ya bajeti ya taifa ili kuhakikisha kuwa jinsi zote zinanufaika.

## Haki za Wanawake:

35. Tanzania imekubali na kuridhia Mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake (CEDAW (1987) na vile vile inaheshimu haki za wanawake kama haki za binadamu. Licha ya kuwa Katiba ya nchi inatambua haki za raia wote bado wanawake kama walivyo wananchi wengi, hawajui haki zao na namna ya kuzitafuta. Hii inatokana na sheria hizo kuandikwa kwa lugha ya kigeni na ya kisheria. Hivyo sheria na taratibu haziwafikii wananchi walio wengi na vile vile ufuatiliaji wa karibu wa sheria na taratibu hizo hukosekana k.m. Sheria ya Ndoa ya 1971 na sheria za mirathi. Baadhi ya sheria za kimila zilizojengeka katika siku za karibuni zimeelekea kuwabagua na kuwakandamiza wanawake. Kwa bahati mbaya upo mkanganyiko katika matumizi ya sheria za Serikali na matumizi ya sheria za kimila na desturi. Katika mkanganyiko huo wanawake wameendelea kubaguliwa na kukandamizwa.

## Mikakati ya Utekelezaji wa Haki za Wanawake

36. Ili kuondoa hali hiyo, mikakati ifuatayo ni muhimu iwekwe:

- Sekta zinazoshughulika na sheria zidurusu sheria zote zenye ubaguzi wa kijinsia kwa mfano Sheria ya Mirathi, na Sheria ya Ndoa (1971).

- Kuhakikisha kuwa wanawake wanashirikishwa katika uongozi wa ngazi zote.
- Kuelimisha wanawake na jamii kuhusu haki za kisheria zinazowagusa.
- Kuelimisha jamii juu ya uwiano mzuri wa kazi za nyumbani kati ya watoto wa kike na wakiume ili kutoa muda wa kutosha kwa watoto wa kike kujisomea.
- Kuhamasisha jamii juu ya uwekezaji katika viwanda vidogo hasa vya kusindika mazao vijijini ambavyo vinaweza kutoa ajira kwa wanawake ambao mara nyingi hawana mitaji mikubwa.
- Kutoa mafunzo na ushauri ili kuwawezesha wanawake kuendesha shughuli zao katika ajira isiyo rasmi kwa ufanisi na faida.
- Kuhamasisha kupiga vita rushwa sehemu za kazi ili kuboresha maadili ya kazi na ufanisi.
- Kuunda chombo cha wanawake kisichofungamana na itikadi ya chama chochote cha siasa kitakachokisaidia kuratibu shughuli za maendeleo ya wanawake ikiwa ni pamoja na kuishauri serikali ipasavyo.
- Kuhakikisha kuwepo kwa uwazi na ukweli katika mfumo wa uwajibikaji katika ngazi zote za serikali.
- Kuimarisha uongozi katika taasisi zote zinazosimamia matumizi ya mali za umma.

## Hali ya Hifadhi ya Jamii

37. Katika nchi yetu bado hapajakuwepo mfumo wa kutosheleza wa hifadhi ya jamii unaowahudumia wananchi wote hasa walioko vijijini, wasioajiriwa na walioko katika sekta isiyo rasmi. Kutokana na hali hiyo wanawake ndio watakaoathirika zaidi endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa kuhakikisha kuwa hifadhi za jamii zilizopo na zinazoamrishwa zinalenga sehemu kubwa ya jamii hasa iliyoko vijijini. Aidha kuna haja ya kuanzisha hifadhi za jamii katika ngazi zote.

## Mikakati ya Hifadhi ya Jamii

38. Ili hali ya hifadhi ya jamii iweze kuhudumia wananchi wengine sawasawa na wanavyohudumiwa wafanyakazi walio katika ajira rasmi, sera itahakikisha kuwepo kwa mfuko wa hifadhi ya jamii katika ngazi za chini. Wahusika wakuu watakuwa ni Halmashauri za wilaya na miji na wananchi wenyewe. Jukumu la Serikali ni kuwezesha Halmashauri hizo kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

## Wingi na Uzito wa Kazi walizonazo Wanawake

39. Katika Tanzania wanawake, hasa wa vijijini hufanya kazi nyingi na nzito na hawapati muda wa kutosha kujiendeleza, kupumzika na wala kujiburudisha. Hali hii huathiri sana afya zao. Wingi wa kazi hizo unatokana na majukumu

mengine waliyonayo ambayo ni pamoja na kuzaa na kulea watoto, kutunza familia, kazi za nyumbani, kulima na kuchangia katika shughuli za uzalishaji.

Aidha uzito huo wa kazi unatokana na mila na desturi, mgawanyo mbaya wa kazi katika familia unaohusishwa na maumbile ya mtu. Vile vile unatokana na kutokutumia teknolojia sahihi, zenye kumrahisishia kazi mwanamke ambaye kwa kiasi kikubwa ndiye anayeathirika na mgawanyo wa kazi uliopo.

Sababu zinazoifanya jamii kutotumia teknolojia sahihi ni pamoja na; kutokufahamu kuwepo kwa teknolojia zinazopatikana hapa nchini, gharama kubwa za usambazaji, uwezo mdogo wa kuzipata kutokana na gharama ya baadhi ya teknolojia hizo kuwa juu sana, wananchi kukosa utaalam wa kuzifanyia matengenezo zinapoharibika, kukosekana kwa teknolojia ambazo zimebuniwa kwa kuzingatia uwezo na maumbile ya watumiaji na kutokuwepo kwa baadhi ya teknolojia.

40. **Mikakati ya Kupunguza Uzito wa Kazi**

- Kuwepo mipango ya kitaifa ya kuwapunguzia wanawake uzito wa kazi
- Jamii ielimishwe juu ya teknolojia mbalimbali zinazopatikana hapa nchini
- Kuwepo utaratibu mzuri wa kupatikana, kusambaza na kutoa mafunzo juu ya

utengenezaji, uendeshaji na utunzaji wa teknolojia.

- Teknolojia zibuniwe na kusanifiwa kwa kuzingatia uwezo na maumbile ya watumiaji
- Kuimarisha huduma za jamii na vituo vya watoto wadogo, na huduma za afya
- Teknolojia sahihi za kurahisisha upatikanaji na hifadhi ya maji kama: pampu za mkono, visima vya maji, matangi ya maji ya gharama nafuu, n.k. zisambazwe ili kurahisisha upatikanaji wa maji safi na salama.
- Jamii ihamasishwe ili wanaume na wanawake waweze kushiriki katika kufanya kazi zote kulingana na uwezo wao ambazo kwa sasa zinafanywa na wanawake. Fikra za kwamba kuna kazi za wanaume au wanawake peke yao, ziondolewe.

Nishati rahisi na nafuu kama : gesi inayotokana na samadi, mkaa wa mawe, umeme n.k. pamoja na majiko yanayotumia kuni na mkaa kidogo vitumike vijijini ili kupunguza uzito wa kazi ya ubebaji kuni waliyo nao wanawake.

## WAHUSIKA KATIKA KULETA MAENDELEO YANAYOZINGATIA USAWA NA JINSIA

41. Sera ya Maendeleo ya Wanawake inalenga katika kuwapatia wanawake fursa na uwezo zaidi wa kujitegemea. Kwa kuwa wanawake ni sehemu ya jamii, ni dhahiri kuwa maendeleo yao hayana budi kuwagusa wanaume, na kwamba wakati mwingine mafanikio katika azma hiyo yatafikiwa kikamilifu kwa kuwashirikisha wanaume au kwa hatua madhubuti zitakazopaswa kuchukuliwa na wanaume.

42. Kwa kuwa usawa wa kijinsia unahitajika katika maeneo yote ya maendeleo, ni dhahiri kuwa usawa huo utapatikana kwa kushirikisha juhudi na michango ya makundi mbalimbali ikiwemo Serikali; Mashirika yasiyo ya kiserikali, ya hiari; wahisani; mashirika ya dini na hasa wananchi wenyewe, wanawake kwa wanaume. Aidha watekelezaji wakuu wa Sera hii ni familia ambazo ndizo hutoa maamuzi mengi yanayohusiana na mahusiano kati ya wanawake na wanaume kwa kuzingatia mila na taratibu za jamii zetu. Hapo ndipo mtoto wa kike anapoweza kukoseshwa elimu, mwanamke kuachiwa kazi nyingi, kunyimwa haki hata ya urithi na pia ndipo mwanamke anapoweza kukoseshwa mgao wake wa mapato

yanayotokana na jasho lake na wakati mwingine hulazimika kufanya vitendo kinyume na utashi wake ili kuweza kumudu maisha.

43. Kwa kuzingatia kuwa wanaume ndiyo wahimili na wanufaikaji wakuu wa mfumo wa kimila uliopo nchini hivi sasa na pia kwa kuzingatia kuwa wanawake ndiyo wazalishaji wakuu kiuchumi na pia ndiyo wazazi na walezi wakuu wa jamii na hasa familia zetu, Sera hii, kama ilivyo Sera mama ya Maendeleo ya Jamii, inasisitiza kuwa utekelezaji wake utafanywa na watu wenyewe, wanawake na wanaume, na hivyo kuondoa kasoro zilizopo katika mahusiano kati ya wanawake na wanaume katika ngazi zote kuanzia familia, ukoo, Serikali za vijiji hadi ngazi ya Taifa.

Aidha, Sera hii inakumbushia kuwa mila na desturi zetu huko nyuma zilitilia mkazo sana suala la ulinzi na hifadhi ya watu wote katika jamii zetu bila ubaguzi wa kijinsia.

### Jamii yenyewe

44. Sera itawezesha kutambua mchango mkubwa wa wanawake katika maendeleo ya familia, jamii na taifa kwa ujumla kiuchumi, kijamii, kisiasa na katika uzazi, malezi n.k. Aidha, jamii zitawezeshwa pia kutambua na kuthamini kazi wanazozifanya wanawake katika maeneo hayo. Kadhalika jinsi zote zione na kutekeleza wajibu wao ipasavyo katika majukumu ya maendeleo ya

familia, jamii na taifa kwa ujumla; kwa kushiriki ipasavyo katika kazi za maendeleo.

45. Licha ya kuthamini mchango wa wanawake katika maeneo yaliyotajwa, jamii, hususan wanaume watawezeshwa kupenda, kuheshimu na kutoa haki sawa na wajibu sawa. Badala ya kuona kuwa kumsomesha mtoto wa kike si lazima , jamii itahimizwa kuona kuwa elimu kwa mtoto huyo ni muhimu sana kwa sababu baadaye ndiye atakayekuwa na dhamana kubwa na majukumu mengi zaidi katika kuiendeleza familia, jamii na taifa, kwa ujumla, kama ilivyokwishafafanuliwa.

46. Wanawake wenyewe watawezeshwa/ wanapaswa kujiamini zaidi na hivyo kushiriki katika masuala mbali mbali yakiwemo elimu, utawala, siasa na katika kufanya maamuzi mbali mbali. Hali iliyopo sasa ya wanawake kuonekana tegemezi kwa wanaume katika kuamua mambo hata yale ambayo huwagusa au kuwaathiri wanawake wenyewe sharti ibadilike.

47. Jamii, wanawake na wanaume, watawezeshwa kuutambua na kuupiga vita umaskini. Katika azma hiyo licha ya kuzitambua na kuzitumia raslimali zilizopo vizuri zaidi, jamii hazina budi kuchukia uvivu na hivyo kufanya kazi kwa bidii na maarifa zaidi ili kuongeza mapato na kuondokana na umaskini. Aidha, wanawake na wanaume hawana budi kujenga tabia ya kujiwekea akiba kwa madhumuni ya kuwekeza au kuepukana na

janga la njaa na aina nyingine za maafa.

48. Jamii pia zinapaswa kuzitambua na kuzipiga vita mila na desturi zilizopitwa na wakati ambazo huwakandamiza au kuwanyima haki wanawake au wanaume au kusababisha matumizi mabaya ya mali, mazao na rasilimali nyinginezo. Desturi hizo ni kama kuwaachia wanawake kazi nyingi wakati wanaume hawajihusishi na kazi zinazo-ongezea familia zao mapato, tabia ya kuwakeketa wanawake au kutumia rasilimali nyingi katika kucheza ngoma za unyago na jando na kuiacha familia katika hali ngumu ya chakula au kipato. Jamii inapaswa pia kuendeleza tabia ya kutumia mapato yanayotokana na jasho la wazalishaji wote katika jamii kwa shughuli za kimaendeleo, badala ya kutumia kwa anasa zaidi.

49. Jamii nzima zitawezeshwa kupenda na kushiriki katika utawala wa sheria na haki sawa kwa wote. Wanawake na wanaume hawana budi kushiriki katika kuchagua na kuchaguliwa katika uongozi wa maeneo yao au miradi na programu zao mbali mbali. Wananchi watawezeshwa kutambua na kupiga vita rushwa na mambo mengine ambayo yanaashiria kuzuia upatikanaji wa haki sawa kwa wote.

50. Wanawake na wanaume watawezeshwa kuona fahari kujitegemea zaidi katika maisha yao kwa ujumla na hivyo kwa makusudi kabisa wapige vita uvivu na tabia tegemezi. Wananchi hao

watawezeshwa zaidi kiteknolojia ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa kasi zaidi na hivyo kuongeza uzalishaji na tija na pia kupata muda wa kujiendeleza kielimu, kimichezo na kupata muda wa kujipumzisha na kufanya ubunifu wa kimaendeleo.

**Serikali**

51. Serikali Kuu na Serikali za Mitaa zote zina wajibu wa kuweka mazingira mazuri ya kisera na kiutekelezaji wa programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Wakati Serikali Kuu inahusika na uandaaji wa Sera, upatikanaji wa watumishi na wataalam, kusimamia amani na utoaji wa haki, Serikali za Mitaa ni chombo cha kuwawezesha wananchi kushiriki katika kufanya maamuzi, kupanga mipango ya maendeleo na kuitekeleza.

52. Kwa kuzingatia hali halisi ya wanawake nchini, Serikali haina budi kuzifanyia tathmini Sera na sheria mbali mbali ili kufanikisha azma ya kuleta usawa wa kijinsia katika maeneo mbali mbali ya maendeleo, sheria na haki. Aidha, Sera hizo hazina budi kuweka bayana ushiriki wa wanawake na wanaume katika utekelezaji wake na, pia watakavyonufaika nazo. Hali kadhalika inatarajiwa kuwa Sera hizo zitaweka bayana majukumu ya watekelezaji wengine ikiwemo Serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, ya hiari, wahisani, mashirika ya dini, viongozi wa jadi na jumuiya mbali mbali.

53. Kwa kuwa elimu, ujuzi na utaalam ni muhimu katika kuleta maendeleo kwa haraka na kwa ufanisi na kwa kuzingatia kuwa wanawake ni wahusika wakuu katika kuleta maendeleo, Serikali haina budi kuweka sera zitakazohakikisha kuwa wanawake wanapata kipaumbele kinachostahili katika nafasi za elimu na mafunzo. Aidha, Serikali haina budi kuhakikisha kuwa wanakuwepo watumishi wa kutosha wa fani ya Maendeleo ya Jamii ili wawawezeshe wananchi, hususan wanawake, wengi zaidi kushiriki katika masuala ya maendeleo; kupiga vita umaskini, mila na desturi zilizopitwa na wakati, pamoja na kutumia huduma za elimu, afya, maji n.k.

54. Ingawa jukumu kubwa la kuleta maendeleo ni la wananchi wenyewe, serikali haina budi kuwekeza kwa kasi zaidi katika miundo mbinu ili kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi. Upatikanaji wa maji katika umbali unaoelekezwa na Sera ya Maji, matumizi ya nishati mbadala ya kuni na mkaa, kuwepo kwa barabara na vyombo vya usafiri n.k. kutasaidia sana kurahisisha kazi na kuongeza tija. Aidha, Serikali inapaswa pia kuimarisha njia za mawasiliano ili wananchi wazielewe Sera na maamuzi mengine ya Serikali kwa ukamilifu na hivyo kuwezesha utekelezaji wake kwa ufanisi zaidi.

55. Kwa kuzingatia umaskini uliokithiri miongoni mwa wananchi na hasa wanawake, na pia kwa kuzingatia kuwa wananchi hao hawawezi

kutimiza masharti ya mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha, kama vile mabenki, Serikali inalazimika kubuni mbinu na mikakati tofauti itakayowawezesha wanawake kupata mitaji na kushiriki kikamilifu katika mfumo uliopo wa uchumi. Hali kadhalika uongozi katika ngazi mbalimbali hauna budi kuimarishwa ili uwasaidie wananchi katika upatikanaji wa masoko bora zaidi kwa bidhaa zao na hivyo kuwaepusha na wanyonyaji.

56. Katika azma ya kuwawezesha wananchi, hususan wanawake, kujipatia mitaji zaidi na kuwaepusha na kunyonywa, Serikali inayo nafasi ya pekee katika kuwahamasisha wananchi wajiunge katika vikundi vya ushirika na hivyo kuchangiana mitaji yao wenyewe. Vikundi hivyo vinaweza kuwa ushirika wa kuweka na kukopa, ushirika wa uzalishaji mali, ushirika wa biashara au vikundi vya upatu na vya kuchangiana vifaa vya nyumbani au vya ujenzi n.k. Kuhusiana na suala hili Serikali inatarajiwa pia kuhamasisha na kuandikisha mashirika ya hiari mengi yatakayojielekeza katika kuwasaidia wananchi na hasa wanawake kupambana na umaskini na kunyonywa.

57. Kwa kuzingatia kuwa stadi na ujuzi mbalimbali ni muhimu katika maendeleo, Serikali haina budi kuviimarisha Vyuo na Vituo vya Mafunzo kwa wananchi kama vile Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (VMW), Vyuo vya Kilimo na Mifugo; Vyuo vya Afya ya Msingi n.k. Uimarishwaji huo

ulenge katika mitaala, wakufunzi na mazingira ya vyuo vyenyewe yawe ya kuwavutia wananchi. Uwekezaji katika eneo hili utatoa matunda ya haraka katika kuwaimarisha wananchi, na hasa wanawake, kiuchumi, kijamii na hata kiutawala na oganaizesheni.

## Wahisani

58. Serikali iliahidi kuendeleza wanawake kwa kuweka mipango yake bayana. Hata hivyo, kutokana na mzigo mkubwa wa kulipia madeni, uwezo wake wa kutekeleza mipango ya maendeleo na kutoa huduma muhimu unapungua. Kwa msingi huo, wahisani watahamasishwa ili waweze kuisaidia serikali na mashirika ya kujitolea kuendeleza mipango, programu na miradi ya kuendeleza wanawake. Programu na mipango hiyo ni pamoja na ulingo wa utekelezaji wa Taifa, (Platform of Action), Programu ya kuendeleza wanawake na jinsia na mipango mingine katika sekta ya afya, elimu , kilimo, maji n.k.

## Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ya Hiari, Wahisani na Taasisi nyingine

59. Mashirika yasiyo ya kiserikali, ya hiari, wahisani na taasisi mbalimbali yamekuwa msitari wa mbele katika kutoa huduma muhimu za kuleta maendeleo kwa jamii. Jitihada zao zimelenga katika kutoa mafunzo, huduma muhimu za jamii

na hata kuchangia katika kuhamasisha jamii kuweka shinikizo la kuleta mabadiliko katika mambo muhimu kama kukomesha ubaguzi, unyanyasaji na udhalililishaji wa wanawake. Juhudi za mashirika hayo kwa pamoja zimeunga mkono mipango, programu na miradi ya serikali.

Serikali kwa kutambua mchango muhimu unaoweza kutolewa na mashirika haya ilianza kuyasajili upya kwenye miaka ya elfu moja mia tisa na tisini. Yanaposajiliwa mashirika haya huonyesha madhumuni na maeneo wanayotaka kuchangia, na Serikali kwa kuamini kuwa kila shirika linao uwezo katika eneo lake hutoa kibali cha kuendeshea shughuli zao. Nguvu na juhudi zao zitalenga:-

(i) Kuongezea wanawake na wanaume uwezo wa kujiletea maendeleo kwa kutoa mafunzo, stadi na ujuzi.
(ii) Kuhamasisha wanawake na wanaume kuhusu umuhimu wa kujileta maendeleo.
(iii) Kuunga mkono juhudi za Serikali katika kuendeleza jamii kiuchumi, kisheria, elimu, mafunzo na ajira.

## UTEKELEZAJI WA SERA

60. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia utakwenda sambamba na utekelezaji wa Sera nyingine za jumla na za sekta mbali mbali zilizoandaliwa kwa ajili ya kuendeleza jamii ya Tanzania.

61. Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia unaeleza wazi muundo na wajibu wa wahusika mbali mbali katika utekelezaji . Hali kadhalika Sera inaainisha mahitaji katika kujenga uwezo wa kila mhusika na kuelezea mbinu za kuwezesha kuitekeleza.

### Utekelezaji wa jumla wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia

62. Mikakati ya jumla ifuatayo itatumika katika utekelezaji wa Sera hii :-

    (i) Kuweka mazingira mazuri na ya Kudumu yatakayosaidia kuleta uwiano kijinsia kwa kuzingatia yafuatayo:-
    - Uongozi bora katika ngazi zote
    - Kuendeleza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi
    - Kutayarisha mipango madhubuti.

    (ii) Kuwezesha viongozi wa vyama vya Siasa,

Wizara mbali mbali, Mashirika ya umma, binafsi, na yasiyo ya kiserikali, wahisani, mashirika ya dini na jamii kuielewa Sera hii.

(iii) Kuimarisha ujuzi wa watumishi wa ugani na waleta mabadiliko "waraghbishi" katika masuala ya Jinsia.

(iv) Kuwezesha mtu mmoja mmoja au familia kukusanya rasilimali zake na kuzitumia katika maendeleo yake au yao na Taifa kwa jumla.

(v) Kutoa nafasi sawa kwa wanawake na wanaume katika kumiliki ardhi kama rasilimali ya msingi katika kilimo na ufugaji.

(vi) Kuunda na kuimarisha vikundi vya kiuchumi na ushirika wa uzalishaji mali vya wanawake.

(vii) Kuimarisha vyanzo vya mikopo pamoja na kuhimiza mpango wa kuweka na kukopa.

(viii) Kuhimiza uanzishaji wa vikundi vya Ushirika ili kukusanya nguvu na rasilimali zao pamoja kwa ajili ya maendeleo yao ya kiuchumi na kijamii.

(ix) Matumizi mazuri ya rasilimali.

## SURA YA TANO

## MFUMO WA URATIBU NA USIMAMIZI WA SERA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA JINSIA

63. Kutokana na ufafanuzi uliokwishatolewa ni dhahiri kuwa utekelezaji wa sera hii utawahusisha wengi wakiwamo Serikali; mashirika ya hiari; mashirika ya dini; viongozi wa kisiasa na kijadi na watu wenyewe; wanawake kwa wanaume. Ni dhahiri pia kuwa usawa wa kijinsia utapatikana pale watu, katika familia zao, watakapoacha kubaguana, kudharauliana au kukumbatia mila na desturi zinazoendeleza ukandamizaji.

64. Kwa kuzingatia ukweli kuwa utekelezaji wa Sera hii utahusisha juhudi za watu, vyombo, na taasisi mbalimbali, shughuli zao hazina budi kuratibiwa kwa makini ili kuwepo na mwelekeo mmoja ulio sahihi, wenye ufanisi na matumizi bora ya rasilimali. Kama ilivyo mipango na shughuli nyingine za maendeleo nchini mfumo wa uratibu wa utekelezaji wa Sera hii utazingatia miundo mbinu ya utawala na maendeleo iliyopo.

65. Vile vile jitihada zitawekwa ili kuhakikisha kuwa mipango yote ya utekelezaji wa Sera mbalimbali, za kiuchumi na kijamii, haina budi kuzingatia madhumuni na malengo ya Sera hii. Kwa mantiki hiyo, uratibu wa utekelezaji wa Sera hii

utafanyika kupitia halmashauri za vijiji; kamati za maendeleo ya kata; halmashauri za wilaya, miji na manispaa; na sekretarieti za mikoa. Katika ngazi ya Taifa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Tume ya Mipango itaratibu uzingatiaji wa Sera hii, katika Sera za jumla na za kisekta kupitia Vitengo vya masuala ya wanawake na jinsia vilivyoanzishwa na vitakavyoanzishwa katika kila sekta.

66. Kutokana na kuwepo vyombo vingi vinavyojishughulisha na masuala ya wanawake na uwezekano wa kuanzishwa vingine, upo umuhimu wa kuwepo kwa chombo cha wanawake kisichofungamana na itikadi zozote za kisiasa ambacho kitafuatilia shughuli za maendeleo ya wanawake. Chombo hiki kazi yake kuu zitakuwa ni kuishauri Serikali, na vyombo vyenye dhamana ya maendeleo ya wanawake kwa lengo la kuhakikisha usawa na haki unaozingatia jinsia kwa wananchi wote. Chombo hicho kitatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa sheria na kanuni za sera hii na sera zingine pamoja na miongozo itakayotolewa na Serikali.

67. Vitengo vya masuala ya wanawake na jinsia katika sekta, mikoa na halmashauri zote ikiwa ni pamoja na Wizara na taasisi mbali mbali vitaimarishwa na pale ambapo havipo vitaanzishwa ili kuhakikisha kuwa kila Sekta inazingatia masuala ya wanawake na jinsia katika

Sera na programu zake. Vitengo hivyo vitajitegemea na vitafuatilia masuala yanayohusu jinsia, vitatoa ushauri kwa mamlaka ya utendaji katika sehemu inayohusika.

68. Yapo baadhi ya mashirika yasiyo ya Serikali (NGOs) ambayo hupata misaada mbalimbali kutoka kwa wafadhili kama vile fedha na vifaa kwa ajili ya kuendeleza wanawake. Hata hivyo hakuna utaratibu wa kupatia taarifa za misaada hiyo kwa vyombo vinavyohusika na kusimamia utekelezaji wa Sera. Hili linafanya Serikali kutokuwa na kumbukumbu za rasilimali zilizopatikana kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wanawake na jinsia kwa lengo la kuboresha upatikanaji huo. Ili kuliondoa tatizo hilo inafaa pawepo utaratibu kuhakikisha kwamba NGOs zinazohusika na wanawake zinatoa taarifa Serikalini ili kuongeza ufanisi katika uratibu wa utekelezaji wa sera hii.

Mwisho:

69. Utekelezaji wa Sera hii kama utafanywa kwa ufanisi utaihakikishia Tanzania maendeleo, usawa na amani kama inavyofafanuliwa katika ulingo wa utekelezaji wa Beijing. Pasipo maendeleo, usawa na haki, amani haitaweza kudumishwa, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya Watanzania.

70. Sera hii ambayo imezingatia Sera mama ya

Maendeleo ya Jamii imezingatia pia mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kimfumo yanayoendelea nchini. Kwa mantiki hiyo mafanikio ya Sera hii yatategemea sana:-

(i) Mchango wa kila Mtanzania katika kutekeleza majukumu yake katika jamii.
(ii) Mafanikio ya utekelezaji wa Sera nyingine k.m. Sera ya Maendeleo ya Jamii, Kilimo, Lishe, Elimu, Utamaduni, Afya, Maendeleo ya Watoto, Viwanda, na Sera zingine zote zitakazo andaliwa kwa ajili ya kuendeleza Jamii ya Tanzania. Aidha itabidi sera zote ziangaliwe upya ili ziendane na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 kuhusu masuala ya maendeleo ya wanawake na jinsia.
(iii) Kuweko na ufuatiliaji na usimamizi wa karibu.

71. Mwisho, Sera hii ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia Tanzania (2000) inachukua nafasi ya Sera ya Wanawake Katika Maendeleo ya Mwaka 1992 ambayo kwa maelezo yaliyotangulia imepitwa na wakati. Lengo ni kuwaendeleza wanawake kwa kutumia dhana ya jinsia. Aidha Sera hii itachangia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Sera Mama ya Maendeleo ya Jamii ambayo imeweka kipaumbele elimu ya kuwawezesha watu kutambua uwezo, fursa zilizopo na rasilimali walizo nazo na kuzitumia kujiletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.